



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

**TAARIFA MUHIMU KWA UMMA KUHUSU MWENENDO WA UGONJWA WA
EBOLA**

Dodoma, 21 Oktoba 2026

Ndugu Wananchi,

Wizara ya Afya inapenda kuendelea kuufahamisha umma kuhusu kuendelea kuwapo kwa tishio la ugonjwa wa Ebola. Tishio hili ni kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Ebola unaoendelea kwenye nchi ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), na hivi karibuni kupatikana kwa mgonjwa wa Ebola nchini Kenya aliyesafiri akitokea DRC.

HATA HIVYO, HADI SASA HAKUNA UGONJWA WA EBOLA NCHINI TANZANIA.

Ndugu Wananchi,

Ugonjwa wa Ebola huambukizwa kwa kugusa majimaji ya mwili wa mgonjwa wa Ebola au mtu aliyefariki kwa ugonjwa huo kama vile damu, mkojo, mate, matapishi, jasho au kugusa vitu walivyovitumia. Vilevile, ugonjwa huu unaweza kuambukizwa kwa kugusa wanyama pori wenye maambukizi kama vile popo na jamii ya sokwe au mizoga yao. Dalili za Ebola ni pamoja na homa, uchovu wa mwili, maumivu ya misuli, maumivu ya kichwa, kutapika au kuharisha. Baadhi ya wagonjwa wanaweza kuonesha dalili ya kutokwa damu sehemu mbalimbali za mwili kama vile puani, machoni, masikioni, njia ya haja kubwa au ndogo.

Ndugu Wananchi,

Serikali imeendelea kuimarisha utayari wa kukabiliana na Ebola kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo: kuimarisha uchunguzi wa afya kwa wasafiri katika viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu; kufuatilia taarifa za wagonjwa katika jamii na vituo vya kutolea huduma za afya; kuimarisha utayari wa vituo vya kutolea huduma za matibabu, upatikanaji wa dawa, vifaa kinga na tiba pamoja na kuwajengea uwezo wataalam ili kutoa huduma kwa wagonjwa endapo ugonjwa huu utaingia nchini; na kutoa elimu kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali. Hali kadhalika, Serikali imeimarisha uchunguzi wa afya kwa wasafiri katika viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu.

Aidha, Serikali imehuisha na kusambaza mwongozo wa wasafiri [Namba 18](#) wa tarehe **17 Oktoba 2026** unaoelekeza hatua za afya zinazopaswa kuzingatiwa na wasafiri wote wanaoingia nchini.

Ndugu Wananchi,

Ili kuifanya nchi yetu kuendelea kuwa salama, kila mmoja wetu ana mchango mkubwa katika kujilinda, kuilinda familia yake na jamii kwa ujumla dhidi ya tishio la ugonjwa huu. Hivyo, Serikali inaendelea kutoa rai na kusesitiza kila mmoja kuzingatia yafuatayo:

- i. Kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni, au kutumia vitakasa mikono (Sanitizers);

- ii. Kuepuka kugusa majimaji ya mwili wa mtu mwenye dalili zilizotajwa hapo awali, au aliyefariki kwa dalili zinazofanana na za Ebola, au kugusa vitu walivyovitumia;
- iii. Kuwahi katika kituo cha kutolea huduma za afya kilicho karibu endapo utakuwa na dalili zinazofanana na za ugonjwa wa Ebola;
- iv. Kutoa taarifa kwa kupiga simu bila malipo kupitia namba 199 endapo utamuona mtu mwenye dalili zinazofanana na za ugonjwa huu;
- v. Kushirikisha wataalam wa afya katika usimamizi wa mazishi ya mtu aliyefariki kutokana na dalili zinazofanana na za Ebola;
- vi. Kuzingatia mwongozo wa wasafiri [Namba 18](#) uliotolewa na Wizara ya Afya mnamo tarehe **17 Octoba 2026**, unaoelekeza hatua za afya zinazopaswa kuzingatiwa na wasafiri wote wanaoingia nchini;
- vii. Kuepuka kugusa wanyama pori kama vile popo na jamii ya sokwe au mizoga yao; na
- viii. Kuendelea kufuatilia taarifa kutoka vyanzo rasmi vya Serikali ili kupata taarifa sahihi, ili kuepuka upotoshaji.

Aidha, **nawasisitiza watoa huduma na watumishi wote wa afya nchini kuendelea kuimarisha utayari wa kutambua mapema dalili zinazoweza kuashiria Ebola**, kutoa taarifa kwa wakati, na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa miongozo ya Wizara ya Afya. **Kwa kuwa wahudumu wetu wa afya mpo mstari wa mbele katika kuwahudumia wagonjwa, mnapaswa kuzingatia kikamilifu kanuni za kuzuia na kudhibiti maambukizi (IPC), ikiwemo usafi wa mikono na matumizi sahihi ya vifaa vya kujikinga kulingana na tathmini ya hatari, ili kujilinda, kuwalinda wagonjwa, na kuzuia kuenea kwa maambukizi.**

Mwisho, nawashukuru tena wananchi wote kuendelea kuzingatia maelekezo ya wataalam na ninawasihi kuendelea kutoa ushirikiano kwa wataalam wa afya wakati wa kutekeleza afua mbalimbali dhidi ya tishio la ugonjwa wa Ebola, ili tuendeleo kuwa salama. Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa ugonjwa huu nje ya mipaka na kuchukua hatua zote muhimu ili kuimarisha usalama wa afya nchini, na itaendelea kuushirikisha umma hatua kwa hatua. Tuendeleo kijilinda na kuilinda nchi yetu.

Imetolewa na;

Prof. Bruno Fokas Sunguya

MGANGA MKUU WA SERIKALI